




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO**



Kumb. Na. BDC/A.2/01/58

23/05/2022.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo anawatangazia wataanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo kuomba nafasi za kazi zifuatazo:-

1. MTENDAJI WA KIJIKI III –NAFASI 12

Sifa za mwombaji:

1. Awe na elimu ya kidato cha nne
2. Awe na Astashahada/cheti *NTA Level 5* katika moja ya fani zifuatazo (Utawala, Sheria, Elimu ya jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya jamii na sayansi ya jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chyuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
3. Awe tayari kupangwa kwenye Kijiji chochote kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

Kazi za kufanya:

1. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji
2. Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu
3. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
4. Katibu wa mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
5. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika Kijiji
6. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Kijiji
7. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji
8. Afisa masuuli na mtendaji mkuu wa Serikali ya Kijiji
9. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote katika Kijiji
10. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Kijiji
11. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

Ngazi ya mshahara TGS B

2. DEREVA II –NAFASI TATU (3)

Sifa za mwombaji:

1. Awe na elimu ya kidato cha nne
2. Awe na leseni daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kupata ajali
3. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali
4. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza

Kazi za kufanya:

1. Kuendesha gari/magari ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ili kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
2. Kuhakikisha gari na vifaa vyake vipo katika hali nzuri wakati wote
3. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
4. Kutunza na kuandika daftari la safari (log book) kwa safari zote
5. Kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kubaini usalama wa gari
6. Kufanya usafi wa gari
7. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali

Ngazi ya mshahara TGS B**3. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II –NAFASI TATU (3)****Sifa za mwombaji:**

1. Awe na elimu ya kidato cha nne
2. Awe na cheti cha utunzaji wa kumbukumbu NTA Level 5

Kazi za kufanya:

1. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/mafaili yanayohitajika kwa wasomaji
2. Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka
3. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika kwa ajili ya matumiszi ya ofisi
4. Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka nk) katika mafaili
5. Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka taasisi za Serikali
6. Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki katika masjala

Ngazi ya mshahara TGS B**3. KATIBU MUHTASI III- NAFASI NNE 4****Sifa za mwombaji:**

1. Awe na elimu ya kidato cha nne, waliohudhuria mafunzo ya uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu. Wawe wamefaulu somo la hatimkato ya Kiswahili na kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft office, Internet, E-mail na publisher

Kazi za kufanya:

1. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
2. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
3. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake wa kazi, majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za ofisi
4. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisi walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu husika
5. Kusaidia kutunza taarifa, kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za mkuu wake na ratiba ya kazi zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi na kumuarifu mkuu wake wa kazi kwa wakati unaohitajika
6. Kusaidia kufikisha maelezo ya mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu mkuu wake wa kazi kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi wa mkuu wake

Ngazi ya mshahara TGS B

Masharti ya jumla kwa waombaji wote

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na asizidi miaka 45
2. Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo
 - (i) Wasifu binafsi wa mwombaji wa hivi karibuni (Curriculum Vitae) wenye anuani, namba za simu na wadhamini watatu (referees) wa kuaminika
 - (ii) Nakala ya cheti cha kuzaliwa, cheti cha kidato cha nne, vyeti vya taalum (NTA Level 5) na leseni kwa madereva
 - (iii) **Namba sahihi au nakala ya cheti cha kitambulisho cha Taifa -NIDA**
 - (iv) Picha moja ndogo ya hivi karibuni (passport size)
 - (v) Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne/Astahada vya nje ya nchi waambatishe uthibitisho wa NECTA/NACTE
 - (vi) Matokeo ya muda (provisional/testimonials/statement of results) hayatapokelewa
 - (vii) Barua ya maombi iandikwe kwa lugha ya Kiswahili/Kingereza
 - (viii) **Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 05/06/2022 saa 9:30 alasiri**
3. Wale watakoachaguliwa kwa ajili ya usaili ndiyo watakaoitwa
4. Halmashauri haitahusika na gharama za kuja kwenye usaili
5. Maombi yote yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatahughulikiwa

Jinsi ya kutuma maombi

Maombi yote yaandikwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo,
S.L.P 2.
TUKUYU.

Aidha, maombi yote yawasilishwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo kwa mkono au yatumwe kwa barua pepe ded@busokelodc.go.tz na si vinginevyo

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUSOKELO**



Atuvonwe T. Chaula

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO**

**Barabara ya Tukuyu, S. L. P 2 Tukuyu, Simu +255 758 007 740, Nukushi: 025 2957492,
Barua pepe: ded@busokelodc.go.tz, Tovuti: www.busokelodc.go.tz**